

Darasa 2

# Wakati wa likizo



Tusome Early Literacy Programme

# Wakati wa likizo



Kato na Amina wanaishi mjini na wazazi wao.

Baba yao hufanya kazi viwandani.

Wakati wa likizo, mama yao aliwapeleka mashambani kuwatembelea jamaa zao.

Amina na Kato walijawa na furaha tele.





Walipofika mashambani, walimkuta babu yao akilisha ng'ombe na mbuzi wake.

Walifurahi sana kumuona babu.

Babu alimshika bata na kuwachinjia Amina na Kato.

Aliwapakulia kitoweo kitamu kwenye bakuli lililokuwa kubwa sana.







Jioni, baba yao mdogo alifika nyumbani kwa babu.

Aliwapeleka Kato na Amina kuwachukua mbuzi wake kutoka malishoni.

Wakati wa jioni, shangazi yao aliwatembelea nyumbani kwa babu.


Shangazi aliwaletea paka wa kuwashika panya.





Asubuhi ilipofika, shangazi aliwapa chai kwa birika.

Pia, aliwapa viazi vitamu kwa sahani safi.



Wakati wa mchana, Amina na Kato walitembea shambani mwa babu.

Waliwaona bata, punda, nguruwe, na mbwa uwanjani.

## Maswali

1. Kato na Amina wanaishi wapi?
2. Babu alikuwa akifanya nini shambani?
3. Kato na Amina walichinjiwa nini na babu yao?
4. Kato na Amina walipelekwa wapi na baba mdogo?
5. Kato na Amina waliona nini uwanjani?

# Wakati wa likizo

Kato na Amina wanamtembelea babu yao wakati wa likizo. Wanapofika wanakaribishwa na kitoweo cha bata. Je, wataona nini shambani mwa babu?

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa 2

# Shangwe uwanjani



Tusome Early Literacy Programme

# Shangwe uwanjani



Leo ni siku ya mashindano ya mpira shuleni.

Darasa la kwanza linashindana na darasa la pili.

Hawa ni watoto wa darasa la kwanza.
Wamevalia sare za manjano.
Viatu vyao ni vyeusi.





Wanafunzi wa darasa la pili wamevalia sare nyekundu.


Viatu vyao ni vya samawati.

Wanafunzi wa darasa la tatu wanapeleka meza uwanjani.

Wengine wamebeba vitabu na kalamu kwenye visanduku.

Vitabu na kalamu ni zawadi za washindi.






Mwalimu mkuu ndiye anaongoza mashindano haya.

Amevalia sare ya rangi ya kijani kibichi.

Walimu wameketi kando ya uwanja.

Mwalimu wa darasa la kwanza amevalia shati nyeusi.





Mashindano yanaanza saa nne kamili.
Wanafunzi na walimu wanashangilia.



Mashindano yanakamilika saa tano na nusu.

Wanafunzi wanapewa vitabu, kalamu na vifutio kama zawadi.

## Maswali

1. Wanafunzi wa darasa la kwanza wamevaa sare za rangi gani?
2. Wanafunzi wa darasa la pili wamevalia viatu vya rangi gani?
3. Wanafunzi wa darasa la tatu wanafanya kazi gani?
4. Sare ya mwalimu mkuu ni ya rangi gani?
5. Wanafunzi walituzwa zawadi zipi?

# Shangwe uwanjani

Darasa la kwanza linashindana na la pili. Timu zote zimevalia sare maridadi. Je, ni darasa lipi litashinda?


USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa 2

# Lishe bora



Tusome Early Literacy Programme

# Lishe bora



Chakula hutupa nguvu ili tukue vyema.


Chakula kinachosaidia mwili huitwa lishe bora.


Lishe bora ni mchanganyiko wa vyakula mbalimbali.

Ni haki ya kila mtoto kupata lishe bora.

Lishe bora huzuia mtoto kupata virusi vya magonjwa mbalimbali.

Vyakula hivi hutoka kwa wanyama au mimea.






Wanyama hutupatia nyama, mayai na maziwa.

Ni vyema kuhakikisha kwamba nyama imepikwa na kuiva kabla ya kuila.

Pia, hakikisha kwamba maziwa yamechemshwa kwa sufuria safi ili kuepukana na minyoo.

Mimea hutupatia vyakula vya aina nyingi sana.

Kuna vyakula vinavyotolewa kwenye mizizi ya mimea kama vile viazi vikuu na mihogo.

Vyakula kama vile: maharagwe, mahindi, ngano na mboga hutolewa kwenye mimea inayokuzwa shambani.





Mimea pia hutupatia matunda kama vile: machungwa, maembe, tikiti na ndizi.

Matunda hutupatia madini yanayozuia magonjwa.

Vilevile, madini husaidia mwili kupona haraka unapougua.

Nyanya ni aina ya tunda.

Nyanya pia hutumiwa kama mboga.

Ni vyema kuosha nyanya kwa maji safi unapotayarisha chakula.





Mboga mbalimbali ni aina za mimea.

Mifano ya mboga ni kama sukumawiki, karoti, vitunguu, mchicha na kabeji.

Ni muhimu kula karoti kwa sababu ina manufaa kwa macho yetu.




Je, utatayarishaje lishe bora?

Changanya vyakula mbalimbali kwa kiwango kinachostahili.

Kwa mfano, tayarisha nyama, mboga, ugali na matunda upate lishe bora!

## Maswali

1. Chakula kinachosaidia mwili huitwaje?
2. Lishe bora husaidia mtoto vipi?
3. Wanyama hutupatia vyakula gani?
4. Taja aina nne za mboga.
5. Eleza jinsi ya kutayarisha lishe bora.

# Lishe bora

Kuna vyakula vya aina nyingi. Ni vyema kula chakula bora ili kuuwezesha mwili kukua vyema. Soma hadithi hii uelewe ni chakula kipi kiitwacho lishe bora.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa 2

# Mzee Kichwa aita mkutano



Tusome Early Literacy Programme


# Mzee Kichwa aita mkutano




Siku moja Mzee Kichwa aliita mkutano. Alitaka kusikiza malalamiko ya sehemu za mwili.

Mkutano ulikuwa kwake nyumbani kwenye kivuli cha mti.

Mzee Kichwa alianza kwa kumwita Jicho. Jicho alilalamika kuwa alisaidia binadamu kila mara lakini hakupata msaada wowote. Mzee Kichwa akamkumbusha Jicho kwamba hupata msaada kwa kulala usiku mzima.





Naye Kidevu akalalamika kuwa binadamu humnyoa kila wiki.


Shavu aliposikia hivyo akasema kuwa ana furaha kwani hapati chawa na vipele.

Hii ni kwa sababu binadamu humnyoa kidevu kila mara.

Kisogo akasema kuwa amewekwa nyuma na kusahauliwa.

Uso akamjibu kwa haraka kuwa yafaa afurahie hali yake. Yeye amelindwa kutokana na maovu.

Uso pia, akalalamika kuwa yeye huchoka kwa kubeba Kinywa, Pua na Macho.





Kidole naye akasema kuwa hufanyishwa kazi nyingi na wakati mwingine chafu.

Kichwa akamwambia kuwa anafaa kushukuru kwani husafishwa mara kwa mara.

Kichwa akamkumbusha kuwa hupokea chakula kabla ya wengine wote.

Pua alilalamika ya kuwa yeye hunusa hewa isiyo safi mara kwa mara.

Hewa hiyo humletea mafua.

Aliomba anunuliwe kitambaa cha kutolea makamasi kila wakati.





Mzee Kichwa aliposikia yote hayo, aliwaambia wote wachukue muda kufikiria mambo ambayo ni mazuri kuhusu maisha yao.

Aliwaambia kuwa yeye hubeba uso, nywele, masikio, kinywa na pua bila kulalamika.

Akasema kuwa yeye huwaongoza wote kwa furaha.



Wote walitazamana kwa aibu.

Kila mmoja akafikiria yote mazuri kujihusu. Wakamshukuru Mzee Kichwa kwa kuwashauri vyema na kila mmoja akaenda zake.

## Maswali

1. Mkutano ulioitwa na Mzee Kichwa ulikuwa wapi?
2. Jicho alilalamika kwa kufanya kazi gani?
3. Taja mambo mawili ambayo kidole hupata.
4. Unafikiri kwa nini kichwa ndiye hufanya kazi nyingi kuliko wote?
5. Taja sehemu tatu za mwili ambazo hazikufika mkutanoni.

# Mzee Kichwa aita mkutano

Kichwa anaita sehemu zingine za mwili kwenye mkutano. Sehemu hizi zinalalamika kwa kazi wanazozifanya. Je, Mzee kichwa anayapi ya kuelezea?


USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa 2

# Mkulima hodari



Tusome Early Literacy Programme

# Mkulima hodari



Tete anaishi katika kijiji cha Panda Mbegu.

Tete ni mkulima aliye na bidii sana.

Anajulikana kijijini kote kwa umaarufu wake katika ukulima.

Tete hupanda mimea mbalimbali na kufuga wanyama pia.

Ng’ombe, kondoo na mbuzi hupatikana katika shamba lake.

Mbali na hayo, Tete hufuga nyuki.





Msimu wa mvua unapofika, Tete hutayarisha shamba lake.


Kwanza, hukata miti iliyo shambani akitumia panga na shoka.


Kisha, hufyeka nyasi akitumia fyekeo.

Shamba lake ni kubwa sana na hulilima kwa kutumia trekta.

Tete hulima shamba lake mara mbili ili kulainisha mchanga.

Kisha, hutoa mabaki ya nyasi na mimea akitumia reki.





Baada ya kulima shamba, Tete hutumia trekta yake kupanda mahindi.

Kazi ya kupanda huchukua siku nzima.

Tete hufurahi sana akimaliza kazi shambani.

Baada ya kupanda mahindi, Tete huanza kazi katika shamba la mboga.

Shamba la mboga liko kando ya lile la mahindi.

Mboga zake hukua vizuri.





Siku moja Tete alikuta viwavi wamevamia mboga yake.

Alikasirika kwa sababu ya hasara aliyopata.

Mazao ya mboga hayakuwa mazuri.

Viwavi ni hatari kwa mimea.
Wao hula majani na kuharibu mimea.
Tete alinunua dawa ya kuwaangamiza.






Tete huzingatia usafi katika boma la wanyama.

Kila wiki, Tete hutia dawa ya wadudu katika zizi la ng’ombe.


Tete hapendi wanyama wake waangamizwe na viroboto.

Tete hupalilia mahindi yake mara mbili na kutia dawa.

Dawa huwaangamiza wadudu na kutoa kwekwe.

Tete amewaajiri wafanyakazi wawili wanaomsaidia shambani.





Tete hupata mapato mengi kutoka kwenye shamba lake.

Ng’ombe na mbuzi wake hutoa lita nyingi za maziwa.

Yeye huuza maziwa sokoni.



Majirani wa Tete humpenda sana.

Wao huenda kwake kupata ushauri kuhusu ukulima.

Tete hufurahia kuwaelimisha watu kuhusu kilimo bora.

## Maswali

1. Tete ni maarufu kijijini mwake kwa kazi gani?
2. Tete hufuga wanyama wa aina gani?
3. Tete hutumia vifaa gani kutayarisha shamba lake?
4. Taja aina tatu ya wadudu ambao humsumbua Tete katika ukulima wake.
5. Ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na ukulima wa Tete?

# Mkulima hodari

Tete ni mkulima hodari katika kijiji cha Panda Mbegu. Yeye hutumia vyombo vya kisasa kulimia. Tete huwapatia majirani wake mawaidha ya kilimo bora.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa 2

# Hali ya hewa nchini



Tusome Early Literacy Programme

# Hali ya hewa nchini




Mutembei anasoma katika shule ya Msingi ya Charia.

Shule ya Charia iko sehemu za Meru, kwenye maeneo ya baridi.

Kila siku akienda shuleni, Mutembei huvaa suruali ndefu, shati na sweta.

Ni lazima kila mwanafunzi avae sweta, soksi na viatu.

Siku moja, wanafunzi wa shule ya Charia walipelekwa kutembelea Jiji la Mombasa.

Mutembei alikuwa na furaha sana, kwani ndoto yake ya kuzuru pwani ilitimia.

Aliwaambia wazazi wake wampangie nguo zake kwenye sanduku.

Mama yake alimsindikiza hadi shuleni.





Wanafunzi walianza safari ya kwenda Mombasa.

Hali ya hewa ilianza kubadilika wakiwa safarini.

Kutoka Meru hadi Nairobi kulikuwa na baridi sana.

Walipofika Salama, hali ya hewa ilibadilika na kukawa na joto tele.

Iliwabidi wanafunzi kuvua sweta zao na kubaki na shati au blauzi.

Wanafunzi walipofika Mombasa, walifurahi kukutana na watu tofauti tofauti.

Walitambua kuwa mavazi huwa tofauti katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Watu wengi wa pwani walikuwa wamevaa nguo nyepesi majira ya joto.

Wakati wa kuogelea, Mutembei alifurahi kubadilisha na kuvaa mavazi ya kuogelea.





Mutembei alishangaa kuona watu wamevalia tofauti na mazoea yake.

Watalii wengi walikuwa wamevaa fulana na kaptula pekee.

Wanawake wengi walikuwa wamevaa buibui, veli na leso.


Marinda mengi ya wanawake yalikuwa mepesi.

Mutembei alikuwa na maswali mengi ya kuuliza mwalimu wao.

Alitaka kujua ni kwa nini watu wa Mombasa huvalia nguo nyepesi.

Mwalimu alimueleza ni kwa sababu ya joto.

Alimueleza joto hilo hutokana na hali ya anga Mombasa.






Mwalimu wao aliwakusanya wanafunzi wote pamoja.

Akawaelezea hali ya hewa katika maeneo mbalimbali ya nchi ya Kenya.

Kwa mfano, pwani mwa nchi huwa na joto jingi kuliko Bonde la Ufa.

Wakenya huvaa mavazi tofauti kulingana na hali ya hewa.

Katika nchi nzima, miezi yenye joto ni Disemba hadi Machi.

Wanaume huvaa mavazi mepesi kama vile: fulana, kanzu, kaptura, shati na suruali.

Wanawake nao huvaa shuka, kanga au leso, buibui, veli na marinda.

Mavazi ya kuvaa nyakati za jua pia hutegemea tamaduni na dini mbalimbali.





Mvua yenye upepo mkali hupatikana miezi ya Aprili na Mei.

Mavazi ya msimu wa mvua huwa mazito.

Watu mara nyingi huvaa koti nzito, suruali ndefu na sweta.

Hivyo basi, ni muhimu wanafunzi wote wavae nguo za kujikinga baridi wakiwa shuleni.


Mwalimu aliwaeleza kuhusu jiji kuu la Kenya.

Hali ya hewa jijini Nairobi huwa nzuri sana kwa mwaka wote.

Lakini wakati mwingine mvua kubwa ya mafuriko hunyesha.

Wakati kama huo, watu huvaa nguo nzito na kubeba miavuli.





Maeneo ya karibu na bahari, huwa yenye joto sana na pia mvua huwa nyingi.

Kwa mfano, hali ya hewa katika pwani ni ya joto.

Mavazi ya watu wa pwani mara nyingi huwa mepesi.

Mavazi haya ni kama vile shuka, marinda, vilemba na kanga.



Mvua yenye ngurumo za radi hunyesha magharibi mwa nchi.

Mafuriko huwafanya watu wahame na kuelekea milimani.

Si vizuri kujikinga mvua chini ya miti.

Hii ni kwa sababu unaweza kupigwa na radi.

## Maswali

1. Taja jina la mwanafunzi anayezungumziwa.
2. Joto lilipoongezeka wanafunzi walifanya nini?
3. Taja aina tatu za mavazi ambayo watu wa Mombasa huvaa.
4. Kati ya pwani na Bonde la Ufa ni sehemu gani iliyo na joto jingi?
5. Kwa nini watu wa pwani huvaa nguo nyepesi?

# Hali ya hewa nchini

Wanafunzi wa Shule ya msingi ya Charia wanaenda ziara Mombasa. Wakiwa huko, mwalimu wao anawafunza kuhusu hali ya hewa nchini Kenya. Pia, anawashauri kuhusu mavazi mbalimbali yanayovaliwa wakati wa hali za anga tofauti.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa 2

# Kabu aenda mjini




Tusome Early Literacy Programme

# Kabu aenda mjini




Kabu anaishi na
wazazi wake katika kijiji
cha Saba.

Kabu ni kijana mwenye bidii shuleni.

Baba yake anampenda sana.


Baba yake humtuza kwa kumnunulia
zawadi.

Kabu alifanya vyema sana katika somo la Hesabu.

Baba yake alimnunulia saa ya mkono.

Kabu alifurahia zawadi hiyo.

Alimuahidi babake kwamba angefanya bidii zaidi shuleni.





Mbali na kununuliwa saa, alipelekwa mjini.

Siku ya kwenda safari waliamka mapema kujitayarisha.

Kabu alipata kiamshakinywa na kuvaa nguo nzuri.


Waliondoka saa nne asubuhi kuelekea mjini.


Babake Kabu alimwambia kuwa ni muhimu watumie muda vizuri.

Walitaka kutembea pahali pengi wakifika mjini.

Walisafiri kwa gari la baba yake.

Kabu aliketi karibu na dirisha.






Baada ya muda mfupi Kabu aliona alama ya hospitali kando ya barabara.

Alimwuliza baba yake maana ya alama hiyo.

Baba yake alimwambia kwamba hiyo ni alama ya hospitali.

Inaonyesha kwamba kuna hospitali karibu na barabara.


Kabu aliona alama nyingine ya pembe tatu iliyochorwa watoto.

Baba yake alipunguza mwendo. Alama hiyo inaonyesha kivukio cha watoto.

Kulikuwa na shule karibu na barabara.

Watoto huvuka barabara kila mara wakienda na kutoka shuleni.





Baba ya Kabu alimwambia, “Ni vizuri kuwa mwangalifu unapoendesha gari.

Mara nyingi ajali husababishwa na madereva ambao hawasomi kwa makini alama za barabara.”


Safari ilikuwa ndefu. Ilikuwa inaelekea saa sita mchana lakini hawakuwa wamefika mjini.

Baada ya nusu saa, baba yake Kabu alisimamisha gari.

Kabu aliona milima na wanyama.

Pundamilia walikuwa wakila nyasi kando ya barabara.

Wanyama hao walikuwa na rangi za kupendeza.






Walianza mwendo baada ya kupumzika.

Waliendesha gari kwa kilomita chache wakapata kivukio cha wanyama.

Punde si punde, pundamilia wawili na swara wakatokea.

Babake Kabu alipunguza mwendo ili wanyama hao wavuke barabara.

Walifika mjini saa nane alasiri.
Waliegesha gari lao na kuingia mjini.
Kulikuwa na watu wengi sana mjini.
Mbali na watu, kulikuwa na magari mengi.






Kabu alifurahi kuuona mji.

Baba alimshika mkono na kumtembeza barabarani.

Alimfundisha jinsi ya kuvuka barabara.

Walitembea mpaka kwenye kivukio cha watu ili waivuke barabara.




Kabu alitembezwa na baba yake mjini.
Ilipofika saa kumi, walienda katika mkahawa kula chakula.
Waliingia kwenye gari lao, kisha wakaenda nyumbani.
Ilikuwa siku ya furaha kwake Kabu.

## Maswali

1. Taja jina la kijiji anamoishi Kabu.
2. Baba yake Kabu alimnunulia zawadi gani?
3. Alama ya pembe tatu aliyoiona Kabu ilichorwa nini?
4. Ajali nyingi barabarani husababishwa na nini?
5. Kwa nini dereva anafaa kuendesha gari polepole mjini?

# Kabu aenda mjini

Kabu ni kijana mwenye bidii shuleni. Baada ya kufanya vyema katika somo la Hesabu, baba yake alimpeleka mjini. Njiani na mjini, Kabu aliona vitu tofauti.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa 2

# Wanamichezo



Tusome Early Literacy Programme

# Wanamichezo




Kiplimo ni mwanariadha hodari.

Ameshiriki katika mbio za aina nyingi na kila mara hupata medali ya dhahabu.

Kila asubuhi yeye huamka mapema sana.

Kisha anaelekea uwanjani.

Akifika kwenye uwanja yeye hukutana na kocha wake.


Kocha wa Kiplimo anaitwa Mutua.

Mutua humwagiza Kiplimo kufanya mazoezi ya misuli.

Daktari wa timu ya Kiplimo huwa tayari anapohitajika.

Kiplimo na wanariadha wenzake huanza kwa mazoezi ya kurukaruka.

Baada ya muda, wote huhema na kuhisi joto kiasi.






Wanapomaliza mazoezi ya kurukaruka, huanza mazoezi ya kukimbia.

Wote husimama kwenye mstari na kungoja amri kutoka kwa kocha.

Kocha akishatoa amri, wanariadha hutimua mbio.

Mbio aina tofauti huchukua muda tofauti.

Kiplimo hukimbia kwa kuzunguka kwenye mistari iliyochorwa uwanjani.

Mistari ya riadha imechorwa katika umbo la duara dufu.


Wanariadha huzunguka mistari hii mara nyingi.

Baada ya mbio, wanariadha hupumzika kidogo.

Kisha huendelea na mazoezi ya misuli.

Kiplimo anapenda mazoezi ya misuli.





Baada ya mazoezi Kiplimo pia hupenda kujiunga na rafiki yake Otindo.

Otindo ni mwanakandanda maarufu.

Kiwanja cha kandanda kina umbo tofauti na kiwanja cha riadha.

Kila asubuhi Otindo husimama kwenye lango la bao. Yeye humngojea rafiki yake Kiplimo.

Anapongoja, hupenda kuchukua mpira wake wa mviringo na kufanya mazoezi.


Ingawa Otindo ni mwanakandanda maarufu, angependa siku moja kuwa askari polisi.

Jana, Otindo alikuwa akitazama mistari mbali mbali katika kiwanja cha kandanda.

Michoro mingi ilikuwa ni ya mraba.

Mingine ilikuwa ya pembe tatu.

Uwanjani pia kulikuwa na mchoro wa duara.





Tofauti na mbio za riadha, mchezo wa kandanda una idadi maalum ya wachezaji.

Kila timu ni lazima iwe na wachezaji kumi na mmoja.

Kati yao kuna kapteni na mlinda lango.

Kila mtu katika timu ana sehemu yake ya kuchezea uwanjani.

Sehemu hizi hutofautishwa kwa michoro mbalimbali.

Siku ya Ijumaa timu ya Otindo ilikuwa na mechi muhimu sana.

Ilikuwa mechi ya kuchagua wachezaji bora. Wachezaji hawa watawakilisha kaunti yao katika michezo ya kitaifa.

Otindo na wanakandanda wenzake walifika mapema.

Walimu wa shule jirani pia walikuwepo.

Madereva na maafisa wa serikali pia walifika.





Ilikuwa siku ya kufana sana.

Timu ya Otindo ilishinda timu ya kaunti jirani.

Watu walishangilia kwa kupiga makofi na kuimba.

Mashabiki walianza kuwapandisha wachezaji juu ya mabega.

Waliunda piramidi ya wanadamu ili kuonyesha furaha yao.

Baadaye makocha wa kandanda na wa riadha waliwahutubia wachezaji.

Walisema kaunti hiyo ilifana sana kwa michezo.

Wanariadha na wanakandanda walifanya vyema sana katika mashindano yao.

Mbunge wa sehemu hiyo aliwaahidi wachezaji wote ziara ya kwenda pwani.

Wanariadha na wanakandanda walisikika wakiimba kwa furaha hadi jua lilipotua.





Otindo na Kiplimo walikumbatiana.

Kiplimo akatoa medali yenye umbo la nyota na kumpa Otindo rafiki yake.

Otindo akaichukua kwa furaha na kusema, “Asante sana rafiki. Sasa ni zamu yangu.”

Akatoa medali yenye umbo la mstatili na kumpa Kiplimo.

Baada ya shukrani kila mmoja alielekea nyumbani akiwa na furaha tele.

Otindo alifika nyumbani saa moja usiku.
Alimkuta mama yake akitayarisha chakula cha jioni.



Otindo alimuonyesha mama yake medali aliyopewa na rafiki yake Kiplimo.
Mama yake alimshauri aiweke juu ya kabati.
Medali hiyo ya umbo la nyota ilivutia sana.

## Maswali

1. Kiplimo hucheza mchezo gani?
2. Kocha wa Kiplimo anaitwa nani?
3. Mistari katika uwanja wa riadha ni ya umbo gani?
4. Otindo hucheza mchezo gani?
5. Kiplimo alimpatia Otindo medali ya umbo gani?

# Wanamichezo

Kiplimo na Otindo ni marafiki na wote ni wanamichezo. Kiplimo ni mwanariadha naye Otindo ni mwanakandanda. Siku moja, kaunti yao ilishinda kaunti jirani katika michezo. Otindo na Kiplimo walibadilishana medali zao zenye maumbo tofauti.

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa 2

# Mkulima tajiri



Tusome Early Literacy Programme

# Mkulima tajiri



Kila jioni Karisa na Kaka yake Bakari, humtembelea amu wao Ichingwa.

Ichingwa ana ng'ombe zaidi ya ishirini.

Ana Kondoo zaidi ya mia moja.

Ichingwa amefuga kuku mia tatu na bata thelathini.


Jioni moja, Karisa, Bakari na Juma walimtembelea amu.


Walipofika kwake waliona amu hakuwa na furaha.

Karisa akasema, “Naona amu ana huzuni.”

Juma akasema, “Pengine ni mgonjwa.”

Bakari akasema, “Labda mifugo yake imepotea.”





Vijana wakatembea kwa kasi kuelekea mahali ambapo amu Ichingwa alikuwa ameketi.

“Amu, kwa nini umejishika tama hivi?” Bakari aliuliza.

“Ama mifugo yako imepotea?”

“Ah, msijali vijana, mimi sina neno, shida kidogo tu hapa.”

Ichingwa akasimama na kuwasalimia vijana hao watatu.

Ichingwa akachukua hatua tatu na kusema, “Mimi nimewaajiri wafanyikazi kumi na wanne kunisaidia kazi.”

“Kitambi ndiye mfanyikazi mkuu hapa.”

“Yeye ndiye anayewasimamia wafanyikazi wale wengine kumi na watatu.”

“Tumekaa naye hapa kwa miaka ishirini na mitatu.”

“Kitambi ni mzee, ana watoto watano.”






"Siku tatu zilizopita alipokea simu kuwa mwanawe wa mwisho alikuwa mgonjwa."

"Aliposikia hivyo alichukua mshahara wake wa shilingi elfu kumi."

"Aliondoka kuelekea nyumbani kwake ambako ni karibu kilomita mia nne kutoka hapa."

"Kuondoka kwake kunanitia hofu kidogo."

Juma akauliza, "Kwa nini kuondoka kwake kunakutia hofu?"


Ichingwa akasafisha koo kisha akamshika Juma mkono.


"Hebu njoo nikuoneshe kitu," akasema huku akipiga hatua mbili na Juma kisha akaendelea.

"Unawaona hawa kondoo wa kike?"

"Ndiyo," Juma akajibu.

"Ni wangapi?" Ichingwa akauliza.





“Moja, mbili tatu ...,” Juma akaanza kuhesabu.

“Ni wengi sana Amu, nadhani ni karibu arobaini hivi,” Juma akasema.

“Naam, umekaribia idadi kamili. Hawa kondoo wa kike ni arobaini na saba.”

“Na wote wanatarajiwa kuzaa kwa muda wa siku tano hadi nane hivi.”


“Tunatarajia wanakondoo wengi juma hili,” Amu Ichingwa akasema.

Akaendelea, “Hofu yangu ni kwamba Mzee Kitambi ndiye anayefahamu zaidi jinsi ya kuwalea wanakondoo na mama zao.”

“Sasa ninahofia kondoo hawa wakizaa huenda wakaathirika na kufa.”

“Hiyo itakuwa hasara kubwa sana.”

“Ninatumaini mwanawe atapata nafuu haraka ili arejee kazini.”






Karisa akasema, “Amu, ikiwa utahitaji msaada tutakaa hapa ili kukusaidia.

Tutajifunza jinsi ya kuilea mifugo katika likizo hii ya majuma matatu.”

“Hilo ni wazo bora Karisa,” Amu akasema.

“Bila shaka kila mmoja wenu atapata hela kidogo ya kununulia vitabu. Mtapata ujuzi mkubwa wa kufuga mifugo.

Mkinisaidia hapa nitawapa kila mmoja, shilingi mia moja hamsini kila siku kama shukrani.”

Vijana walifurahi sana.


Kila mmoja wao alikuwa na tabasamu kubwa sana usoni mwake.

Mara moja walitoka wakaenda kuvaa viatu vya kazi.

Juma akamwuliza Bakari, "Tukifanya kazi hapa siku tano kwa wiki tutakuwa na pesa kiasi gani kwa jumla?"

Bakari akasema "Hebu nifanye hesabu... mmmm..."





"Shilingi mia moja na hamsini mara tatu itakuwa ni shilingi mia nne hamsini."

"Sasa, shilingi mia nne hamsini mara tano itakuwa shilingi elfu mbili mia mbili na hamsini!"

"Tutakuwa matajiri sana hapa mtaani!"

"Tutanunua chochote tutakacho."

"Tutanunua viatu vya kisasa."

Karisa akasema, “Nina wazo zuri hapa.”

“Mnaonaje tukimwomba amu atupatie kondoo mmoja kila mmoja wetu badala ya pesa?”

“Tutawauliza wazazi wetu watusaidie kufuga.”

“Mimi ningependa kuwa mfugaji kama amu nikikamilisha masomo.”

“Nitakuwa na mifugo aina mbalimbali.”

## Maswali

1. Mzee Ichingwa alifuga bata wangapi?
2. Mfanyikazi mkuu katika Shamba la Ichingwa alikuwa nani?
3. Ichingwa alikuwa na kondoo wangapi wa kike?
4. Ungependa kupewa kondoo ama pesa? Kwa nini?
5. Karisa na Bakari wakipewa shilingi mia moja na hamsini kwa siku tano kila mmoja wao atapata pesa ngapi?

# Mkulima tajiri

Ichingwa ni amu wa Karisa na Bakari aliye na mifugo wengi. Siku moja, Karisa, Bakari na rafiki yao Juma wanamtembelea amu Ichingwa. Wanampata akiwa na huzuni. Je, ni nini kilichomfanya amu Ichingwa kuwa na huzuni?

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa 2

# Mgeni shuleni



Tusome Early Literacy Programme

# Mgeni shuleni



Mwalimu wetu Bwana Hekima alituita sote. Tukakusanyika mbele ya ofisi yake. Alikuwa na mambo muhimu ya kutueleza sisi na walimu wetu. Bwana Hekima alikuwa na mgeni. Jina la mgeni lilikuwa Bwana Tibabu. Alikuwa amealikwa kuzungumzia magonjwa hatari yanayowasumbua watu.

Bwana Tibabu alianza kwa kuwasalimia walimu na wanafunzi.

Akatushukuru kwa kufika na akatuomba tutilie maanani mambo ambayo angeyasema.

Alisema kwamba kila mtoto ana haki ya kupata habari kuhusu afya yake.

Kwanza, alitueleza kuhusu aina tofauti za homa. Akasema kuwa wakati wa kiangazi hasa kutoka mwezi wa Disemba hadi Machi watu wengi huugua homa.

Homa huletwa na virusi.






Si rahisi kujua aina ya homa unapougua. Unahitaji kwenda hospitalini kupata matibabu.

Ni jambo muhimu kwa kila mtu kupata chanjo kabla ya msimu wa homa. Kuna homa aina nyingine inayoletwa na vimelea.

Kwa kawaida mtu huhisi maumivu katika koo. Kisha watu wengi hukohoa sana.


Unapopatwa na homa aina hii, jaribu kutumia vinywaji vyenye joto, matunda na chakula chenye afya bora.


Hii hupunguza kuenea kwa virusi hivi.

Unapokohoa tumia kitambaa safi kufunika kinywa chako.

Unaposafiri kwa gari, hakikisha madirisha yamefunguliwa. Ukifungua madirisha utapata hewa safi.

Homa hii humfanya mgonjwa kutokwa na kamasi. Ni muhimu kuwa na usafi wa hali ya juu wakati huu ili kupunguza usambazaji wa homa.







Homa nyingine hutokea wakati wa baridi hasa katika miezi ya Juni hadi Oktoba. Aina hii husambaa sana kupitia mikononi tunaposalimiana.

Tunapotumia vyumba ambavyo havina hewa ya kutosha huwa tunaambukizana magonjwa.

Ni vizuri tuwasaidie wazazi na walimu wetu kwa kuyafungua madirisha nyumbani na madarasani.

Ni haki ya kila mtoto kukaa katika chumba chenye nafasi na madirisha ya kutosha.

Hewa safi husaidia kupunguza makali ya homa aina zote.

Bwana Tibabu aliendelea kuongea juu ya magonjwa ya ngozi.


Alisema kuwa ngozi husaidia kufunika mwili wote. Ni muhimu kwa kila mtu kulinda ngozi yake kwa kuisafisha na kuvaa nguo safi.

Lishe bora pia huipa ngozi kinga kutokana na magonjwa mbalimbali.

Kwa mfano, vipele aina tofauti tofauti huchibuka ngozini kutokana na kuumwa na wadudu kama chawa.

Ni muhimu kuwa na nguo na nywele safi kila wakati.






Wakati mwingine vipele hutokea ngozini kutokana na madhara ya vyakula.

Kuna watu ambao huugua wakila mayai, maharagwe au nyama. Mara nyingi daktari huwapa dawa ya kuzuia vipele kutokea kwenye ngozi zao.


Daktari huwashauri kutokula vyakula vinavyofanya waugue. Kila mzazi ana jukumu la kuwatazama watoto wake wasiwe katika hali hii. Walimu pia wanafaa kuwa waangalifu wanapowapatia wanafunzi vyakula shuleni.


Kisha, Bwana Hekima akazungumza juu ya ugonjwa wa malaria. Alisema kuwa ugonjwa huu huenezwa na mbu. Alituhimiza tujihadhari na mbu hasa wakati tunapocheza jioni.

Alitushauri pia tuweze kulala ndani ya vyandarua vilivyotiwa dawa.

Mazingira pia yanafaa kuwa safi bila nyasi ndefu.

Inafaa pasiwe na maji pia yanayosambaa mahali popote.





Mbu hutaga mayai mahali palipo na maji. Tulihimizwa tusaidie katika kusafisha mazingira ya shule yetu.

Hii ni kwa kutafuta na kutoa vyombo vyovyote vinavyoweza kuhifadhi maji.

Wanafunzi wakubwa walitakiwa kuzunguka mazingira ya shule na kufyeka nyasi ndefu.

Walimu walihimizwa kuwapanga wanafunzi katika makundi.


Walitakiwa pia wawe mfano bora kwetu.

Ugonjwa mwingine unaosambaa sana siku hizi ni kipindupindu. Huu ni ugonjwa unaoletwa na uchafu.


Tukisafisha mazingira yetu tutaangamiza kipindupindu kabisa.

Bwana Hekima alituambia kuwa kipindupindu ni ugonjwa wa kuhara, kutapika na kuishiwa na maji mwilini.

Ni vizuri kwenda hospitalini haraka sana ili kutibiwa mtu anapougua. Siku hizi kuna dawa nzuri za kutibu ugonjwa huu.







Mwishowe, Bwana Hekima alizungumza kuhusu ukimwi. Alituambia kuwa hii ni hali ya ukosefu wa kinga mwilini.

Ukimwi hauna dawa lakini madaktari wanajitahidi kuitafuta.

Hivyo, mtu anapopatikana na ugonjwa huu, lishe bora huwa muhimu sana ili kuupatia mwili kinga. Alituhimiza tusiwaogope walio na ukimwi kwani hausambazwi kwa hewa.

Alitushauri pia kuwa ni vibaya kuwabagua wanaougua ukimwi.

Bwana Tibabu aliendelea kusema kuwa kila mtu ana jukumu la kujichunga. Alituhimiza kula vyakula vyenye afya. Ni muhimu kufanya mazoezi kwa njia ya kufanya kazi.

Ni vyema kuwasaidia wazazi wetu katika kazi nyumbani. Hata hivyo, alisema kuwa watoto wasipewe kazi ngumu ili waweze kufanya kazi zinazowafaa.

Tunafaa kujitahidi kwa kusafisha mazingira yetu na kupanda miti ili tupate maji ya kutosha.





Bwana Tibabu alimalizia kwa kuwapongeza tena walimu na wanafunzi.

Baadaye akamwalika mwalimu Hekima. Mwalimu akampongeza Bwana Tibabu na kumsihi arudi siku nyingine.

Pia, alimwahidi kuwa angepanga siku moja kila mwezi, ya kuyasafisha mazingira ya shule.

Kila kundi la wanafunzi litapewa kazi inayofaa. Walimu pia walitakiwa kuyaongoza makundi hayo.

Bwana Tibabu alipoondoka, Mwalimu Hekima aliwaita walimu wote katika mkutano.

Akawaambia wawagawanye wanafunzi wao katika vikundi. Kila darasa liwe na vikundi vya wasichana na vya wavulana.

Wadogo watakuwa katika kikundi kimoja na wakubwa katika kikundi kingine.

Walimu wengine waliambiwa wapange ratiba ya kazi kwa vikundi vyote. Kila mtu alikuwa na kazi ya kufanya.





Walimu walipomaliza, Bwana Hekima alituita tena.

Kila Mwalimu alisoma majina ya vikundi vya darasa lake.

Waliwaita pia viongozi wa vikundi vyao.

Sehemu za kazi ziligawanywa. Kila kikundi kikamwendea mwalimu wao.



Ijumaa ilipofika tuliendelea na masomo hadi saa saba.

Baada ya chakula cha mchana, wanafunzi na walimu walichukua vifaa vya kazi.

Madarasa yakasafishwa. Nyasi zikakatwa. Vyoo vikasafishwa. Sote tulifurahia kukaa katika mazingira safi.

## Maswali

1. Bwana Tibabu alikuwa amealikwa kufanya kazi gani?
2. Unapaswa kufanya nini unaposhikwa na homa?
3. Ni miezi gani ambayo watu huwa na hatari ya kupatwa na homa?
4. Ukimwi ni ugonjwa gani?
5. Tunafaa kufanya nini ili kujikinga na magonjwa mbalimbali?

# Mgeni shuleni

Mwalimu mkuu, bwana Hekima alimwalika bwana Tibabu shuleni. Bwana Tibabu anazungumzia magonjwa hatari yanayowasumbua watu. Bwana Tibabu anawashauri wanafunzi jinsi ya kujikinga kutokana na magonjwa hayo.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 1

Kiswahili

# ★ Shujaa Musa

# ★ Mnyama Nimpendaye



Tusome Early Literacy Programme

# Shujaa Musa

*Mwandishi:* ***Stephen Kwoma***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Katika kijiji cha Matopeni, palikuwa na wawindaji haramu waliokuwa na mazoea ya kuwaua wanyama wa pori. Wanakijiji wa Matopeni walikasirishwa na wawindaji hawa. Wanyama wa pori huwavutia watalii kwenye kijiji cha Matopeni.

Mfalme wa Matopeni aliita mkutano ili kuamua jinsi ya kupambana na wawindaji hao haramu.



Mfalme alipendekeza kuwa, vijana walinde msitu ili wawindaji haramu wasiingie na kuwaua wanyama. Watu wote walifurahia jambo hilo. Walimuunga mfalme wao mkono. Usiku huo, vijana wote waliwangoja wawindaji haramu kando ya msitu. Vijana hao walikuwa na panga, mikuki na mishale. Usiku huo wawindaji haramu hawakutokea.



Usiku wa pili vijana walikuwa wamechoka na wakaanza kusinzia. Wawindaji haramu walitokea. Waliwanyemelea wanyama wa mwituni na kuwaua. Kelele za wanyama ziliwaamsha vijana. Waliwaona wawindaji haramu wakitoroka na mizoga ya wanyama. Vijana waliwafukuza wawindaji hao haramu bila mafanikio.



Mfalme aliitisha mkutano wa pili ili kusuluhisha tatizo hilo. Wakati huu, aliahidi kumtawaza yeyote yule atakayewakamata wawindaji haramu kuwa kiongozi wa kijiji. Wanakijiji walijawa na wasiwasi. Waliogopa kuwa, wawindaji haramu wangewamaliza wanyama pori.



Musa alikuwa mmoja wa vijana waliojitokeza kuwasaka wawindaji haramu. Ingawa alikuwa na umri mdogo, aliandamana na vijana wenzake wakiwa na silaha hatari. Vijana hawa waliwasaka wawindaji haramu wakiwa na panga, mishale, mikuki na hata mbwa wakali. Waliwatafuta wawindaji haramu kwa muda mrefu sana.



Baada ya kuwakosa wawindaji haramu, wengine wao walirudi nyumbani. Musa na wenzake waliamua kuendelea kuwasaka wawindaji haramu. Haikuchukua muda wawindaji wakajitokeza kichakani. "Nyamazeni wawindaji haramu ndio wale," Musa alisema kwa sauti ya chini. Wote walijificha kwenye vichaka.



Musa alimlenga mshale mwindaji haramu mmoja na kumdunga shingoni. Ghafla, yule mwindaji haramu alianguka chini kwa kishindo pu! Wawindaji haramu wengine walitoroka. Musa na wenzake walimbeba yule mwindaji haramu hadi kijijini.



Walipofika kijijini Matopeni walifurahi sana. Walimhoji yule mwindaji haramu ili awaelekeze kwa wale wengine waliotoroka.

Wote walishikwa na kufungwa gerezani.

Kama alivyoahidi, mfalme aliandaa sherehe kubwa sana. Watu walifika kwa wingi kuona Musa akitawazwa. Mfalme alimpa Musa mkuki na ngao. Hapo Musa akatawazwa. Akawa kiongozi wa kijiji cha Matopeni.



Tangu wakati huo, wanakijiji hawakuwa na hofu ya kuuawa kwa wanyama pori tena. Hali ya kawaida ilirejea kijijini Matopeni.

## Maswali

1. Wanakijiji wa Matopeni walikasirishwa na nini?
2. Mfalme aliahidi nini kwa yule angewakamata wawindaji haramu?
3. Taja silaha tatu ambazo vijana walibeba kuwatafuta wawindaji haramu?
4. Ni nani aliyemlenga mshale mwindaji haramu?
5. Mfalme alimpa nini Musa?

# Mnyama Nimpendaye

*Mwandishi:* ***Stephen Kwoma***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Huyu ni mbwa wangu.

Mbwa wangu anaitwa Dora.

Mimi nampenda mbwa wangu.



Mbwa wangu hupenda kula mifupa.


Mimi humpa mbwa wangu mifupa kila siku.

Mbwa wangu huishi kibandani.



Mimi hupenda kutembea na mbwa wangu.

Mimi humfunga mbwa wangu asiwaume wageni.



Mbwa wangu ni safi na hana viroboto.


Mimi humuosha kwa maji safi na dawa.



Mbwa wangu hunilinda usiku.

Mbwa wangu akibweka mimi huamka.

Mbwa wangu hapendi wezi.



Mbwa wangu ni mchangamfu.

Mbwa wangu hupenda kukimbia.

Sisi hucheza na mbwa wangu.



## Maswali

1. Mbwa aliyetajwa kwenye hadithi anaitwa nani?
2. Mbwa hupenda kula nini?
3. Mbwa huishi wapi?
4. Kwa nini mbwa hufungwa?
5. Kwa nini mbwa hana viroboto?

Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 1

# ★ Shujaa Musa

# ★ Mnyama Nimpendaye

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 2

Kiswahili

# ★ Mama Mzee na Nguruwe

# ★ Juma na Sungura



Tusome Early Literacy Programme

# Mama Mzee na Nguruwe

*Mwandishi:* ***Nashera Ara Kodawa***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Hapo zamani za kale palikuwa na mama mzee. Mama mzee aliishi peke yake katika kibanda kidogo.

Siku moja, mama mzee alienda msituni kutafuta kuni.

Alipokuwa akirudi nyumbani, aliokota kipande cha dhahabu.



Alifurahi sana akasema, “Nina bahati sana. Nitaenda sokoni nimnunue Nguruwe.”


Mama mzee alienda sokoni na kubadilisha kile kipande cha dhahabu.

Alipewa Nguruwe mkubwa.

Mama mzee alipofika mtoni akirudi nyumbani, yule Nguruwe alikataa kuvuka mto.



Mama mzee aliomba usaidizi wa Mbwa aliyetokea kichakani, “Mbwa, nakuomba umuume huyu Nguruwe avuke mto. Amekataa kuvuka daraja na hivyo atanifanya nichelewe kufika nyumbani.” Mbwa alikataa kumuuma Nguruwe.



Mama mzee alirudi nyuma kutafuta usaidizi na akaona Fimbo. Akasema, "Fimbo, Fimbo, naomba unisaidie kumchapa Mbwa. Amekataa kumuuma Nguruwe. Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani." Fimbo ikakataa kumchapa Mbwa.



Mama mzee akaendelea kutembea na akaona Moto. Akasema, "Moto, Moto, naomba unisaidie kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe, Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani." Moto ukakataa kuichoma Fimbo.



Mama mzee akaenda akakutana na Maji. Akasema, "Maji, Maji, naomba unisaidie kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe. Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani." Maji yakakataa kuuzima Moto.



Mama akaenda akakutana na Mbuzi. Akasema, "Mbuzi, Mbuzi, naomba unisaidie kuyanywa Maji. Maji yamekataa kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe. Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani." Mbuzi akakataa kuyanywa Maji.



Mama mzee akaendelea na safari yake na akakutana na Kamba.



Akasema, "Kamba, Kamba, naomba unisaidie kumfunga Mbuzi. Mbuzi amekataa kuyanywa Maji. Maji yamekataa kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe.

Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani."

Kamba ikakataa kumfunga Mbuzi.

Mama mzee akaendelea kutembea na akakutana na Panya. Akasema, "Panya, Panya, naomba unisaidie kuitafuna Kamba. Kamba imekataa kumfunga Mbuzi. Mbuzi amekataa kunywa Maji. Maji yamekataa kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe. Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani."
Panya akakataa kuitafuna Kamba.




Mama akaendelea kutembea na akakutana na Paka. Akasema, “Paka, Paka, naomba umle Panya. Panya amekataa kuitafuna Kamba. Kamba imekataa kumfunga Mbuzi. Mbuzi amekataa kuyanywa Maji. Maji yamekataa kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo.

Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe. Nguruwe amekataa kuuvuka mto. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani."
Paka akamwambia mama, "Hiyo kazi nitaifanya lakini kwanza unipe maziwa.



Mama mzee akaenda akakutana na Ng’ombe. Akasema, “Ng’ombe, Ng’ombe, naomba unisaidie maziwa nimpe Paka. Paka amekataa kumla Panya. Panya amekataa kutafuna Kamba. Kamba imekataa kumfunga Mbuzi. Mbuzi amekataa kuyanywa Maji. Maji yamekataa kuuzima Moto. Moto umekataa kuichoma Fimbo. Fimbo imekataa kumchapa Mbwa. Mbwa amekataa kumuuma Nguruwe. Na mimi nitachelewa kufika nyumbani.” Ng’ombe akamruhusu mama mzee kukama maziwa.



Mama mzee akachukua maziwa na kumpelekea Paka. Paka alipokunywa maziwa akashiba, akaanza kumfukuza Panya. Panya akaanza kukimbiza Kamba. Kamba ikaanza kumfukuza Mbuzi. Mbuzi naye akakimbilia Maji. Maji yakaanza kuufuata Moto. Moto ukaanza kuitafuta Fimbo. Fimbo ikaanza kumfukuza Mbwa. Mbwa akaanza kumfukuza Nguruwe.



Nguruwe akauvuka mto kwa haraka na yule mama mzee akafika nyumbani mapema.

## Maswali

1. Mama mzee alienda msituni kutafuta nini?
2. Mama Mzee aliokota nini alipokuwa akirudi nyumbani?
3. Mama Mzee alienda sokoni kununua nini?
4. Kwa nini Mama Mzee alitaka fimbo imchape Mbwa?
5. Ni nani aliyemsaidia Mama Mzee?

# Juma na Sungura

*Mwandishi:* ***Flavia Nanzala***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Hapo zamani paliishi mzee mmoja aliyeitwa Musa. Musa aliishi na mkewe na mwanawe aliyeitwa Juma. Juma alikuwa kijana aliyependa sana kucheza. Hata hivyo, mara nyingi Juma hakuyasikiza kwa makini maagizo ya wazazi wake.

Mzee Musa alikuwa na shamba kubwa la njugu. Siku moja alienda shambani mwake kuvuna njugu. Alishangaa kupata kuwa njugu zilikuwa zimeng'olewa upande mmoja.

Baada ya kuwaza la kufanya, Mzee Musa aliamua kuweka mtego shambani ili amnase mwizi wa njugu zake. Baada ya kuweka mtego, mzee Musa alirudi nyumbani.



Siku iliyofuata, Musa na mwanawe Juma walielekea shambani. Walipofika, Juma alipanda juu ya mti wa mapera kuchuma mapera.

Mzee Musa naye aliendа moja kwa moja hadi pale alipoweka mtego. Lo! Kumbe mwizi alikuwa Sungura. Sungura alikuwa amenaswa kwenye mtego. Sungura alimtazama Mzee Musa kwa jicho la huruma. Sungura alimuomba msamaha.




Mzee Musa alichukua kiboko na kuanza kumcharaza Sungura. Kisha alimchukua Sungura na kumweka ndani ya gunia.

Alimuita Juma na kumwambia, "Mpeleke huyu Sungura nyumbani. Mwambie mama apike kitoweo kitamu cha jioni." Juma hakuyasikiza maagizo ya baba yake kwa makini. Kwani alikuwa akiwalenga ndege mtini.



Juma alichukua gunia lenye Sungura na kuelekea nyumbani. Njiani Sungura alimwuliza Juma, "Je, ulisikiza vizuri maagizo ya baba yako?"

“Alisema, umwambie mama yako amchinje jogoo mkubwa. Akimaliza kutayarisha kitoweo, ampe mgeni ale kisha apumzike.” Juma alimshukuru Sungura kwa kumkumbusha aliyosema babake.



Walipofika nyumbani, Juma alimpa mama yake maagizo hayo ya Sungura. Mama yake alitayarisha chakula akampa Sungura akala. Baada ya kula, Sungura akatoroka.

Baba aliporudi alisema apakuliwe kitoweo. Alishangaa, kwani alitarajia kula nyama ya Sungura. Mama alipomweleza maagizo ambayo Juma alimpa, Musa alikasirika sana. Alimuadhibu vikali mwanawe Juma. Tangu siku hiyo Juma husikiza kwa makini maagizo anayopewa.

## Maswali

1. Baba yake Juma aliitwa nani?
2. Mwizi wa njugu alikuwa nani?
3. Baba yake Juma alimuweka Sungura wapi?
4. Baba yake Juma alitaka Sungura afanyiwe nini?
5. Kwa nini Musa hakuyasikia maagizo ya baba yake kwa makini?

Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 2

# ★ Mama Mzee na Nguruwe

# ★ Juma na Sungura

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 3

Kiswahili

# ★ Fisi na Mbuzi

# ★ Kuku na Mwewe Wakosana



Tusome Early Literacy Programme

# Fisi na Mbuzi

*Mwandishi:* ***Stephen Kwoma***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***


Hapo zamani Fisi na Mbuzi walipendana sana.

Fisi na Mbuzi waliishi pamoja mwituni.

Fisi alikuwa na wana wawili.

Mbuzi pia alikuwa na wana wawili.

Wana wao walicheza pamoja.





Familia za Mbuzi na Fisi zilikula pamoja.

Wanyama hawa walitafuta chakula kwa zamu.

Fisi na Mbuzi hawakufichana chochote.

Siku moja Fisi alipanga njama ya kuwala wanambuzi.

Fisi alifurahi sana Mbuzi alipoenda kutafuta chakula.

Alitafuta kikapu na kuwaweka wanambuzi humo.

Fisi alifurahi sana kwa vile aliona kitoweo kizuri.






Fisi aliwachukua wanambuzi na kuwaficha kichakani.

Baadaye Fisi alirudi nyumbani mbio ili amdanganye Mbuzi.

Mbuzi alipokuwa akirudi aliona kikapu kichakani.

Alichungulia na kupata ni wanawe.

Mbuzi aliwatoa na kuwaficha mahali pengine.



Mbuzi aliamua kurudi nyumbani kwao.

Hakumpata Fisi.

Aliwaingiza wanafisi kikapuni, akawapeleka pale ambapo Fisi alikuwa amewaficha wanambuzi.



Fisi kwa ulafi wake alikimbia kuwala wanambuzi.


Alipofika kichakani alicheka na kusema, "Leo mtanijua."


Fisi alifumba macho na kuwameza wanawe bila kujua.

Fisi alirudi nyumbani akiwa na furaha ya shibe.

Aliwatafuta wanawe lakini hawakuwepo.

Fisi alipoangalia nje alimuona Mbuzi na wanawe wakitoroka.





Fisi alijawa na hasira kisha akawafuata mbio.

Mbuzi na wanawe nao waliongeza kasi.

Mbuzi alipiga mayowe ya kutaka usaidizi.

Binadamu walifika kuona kilichokuwa kikitendeka.

Kwa uoga, Fisi aliwatoroka

binadamu, akajikwaa akaumia mguu.

Mbuzi naye aliokolewa na kupewa makao na binadamu.




Fisi alijutia ulafi wake.

Akaishi akiwa mlemavu.

Mbuzi naye aliishi maisha ya raha na binadamu.

Tangu siku hiyo Mbuzi na Fisi hawapendani.



Fisi bado anamtafuta Mbuzi kulipiza kisasi.

Naye Mbuzi akimuona Fisi hutoroka.

Hicho ndicho kilichokuwa chanzo cha uadui kati ya Mbuzi na Fisi.

## Maswali

1. Fisi alikuwa na wana wangapi?
2. Mbuzi alikuwa na wana wangapi?
3. Kwa nini Fisi alijawa na hasira?
4. Ni nani aliyemsaidia Mbuzi?
5. Mbuzi huishi wapi siku hizi?

# Kuku na Mwewe Wakosana


*Mwandishi:* ***Flavia Nanzala***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Zamani za kale Kuku na Mwewe walikuwa marafiki.

Walipendana sana na hata waliishi pamoja.

Ndege hawa walitaga mayai na kupata vifaranga.



Kuku na Mwewe walikubaliana kuwatunza vifaranga wao kwa zamu.


Mmoja wao alipoenda kutafuta chakula, mwingine alibaki kutunza vifaranga.

Siku moja ilikuwa zamu ya Mwewe kutafuta chakula.

Mwewe aliondoka nyumbani mapema sana.

Kuku na vifaranga walingoja chakula kwa hamu.

Mwewe aliporudi alikuwaameficha chakula chini ya mabawa yake.



Alimdanganya Kuku kuwa alikutana na mbwa njiani.

Mbwa akala chakula chote alichokuwa amekibeba.

Mwewe aliwafunika vifaranga wake na kuwapa chakula.

Kuku na vifaranga wake hawakula chochote siku hiyo.



Siku iliyofuata Mwewe alienda tena kutafuta chakula.

Vifaranga wa Mwewe walikuwa wanacheza kwa furaha.

Vifaranga wa Kuku walilia kwa njaa.

Kuku alishangaa sana.

Aliwauliza vifaranga wa Mwewe ikiwa walikuwa na njaa.

Vifaranga wa Mwewe wakajibu kuwa mama yao aliwaletea chakula.

Wakamwambia Kuku kuwa Mwewe aliwafunika kwa mabawa yake na wakala.



Kuku alikasirika sana. Kwa hasira kuu, alichimba shimo akawafunika vifaranga wa Mwewe. Kisha Kuku na vifaranga wake wakatoroka.

Mwewe aliporudi nyumbani aliwatafuta vifaranga wake lakini hakuwaona. Alipotoka nje, akawasikia vifaranga wakilia kwenye shimo. Aliwatoa kwenye shimo na akaapa kulipiza kisasi.



Hii ndiyo sababu Mwewe hula vifaranga wa Kuku kila anapowapata.

## Maswali

1. Mwewe alificha chakula wapi?
2. Kwa nini watoto wa Mwewe walikuwa wakicheza kwa furaha?
3. Kuku aliwafanyia nini watoto wa Mwewe?

Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 3

# ⭐ Fisi na Mbuzi

# ⭐ Kuku na Mwewe Wakosana

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.


Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 4

Kiswahili

# ☆ Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni

# ☆ Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu



Tusome Early Literacy Programme

# Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni

*Mwandishi:* ***Nashera Ara Kodawa***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Hapo zamani, paka alikuwa rafiki ya Mzee Mkulima. Paka aliishi na Mzee Mkulima na mkewe Malkia. Kila siku baada ya chakula cha asubuhi, paka na Mzee Mkulima waliondoka kwenda shambani kulima na kutafuta chakula.



Paka alishangazwa na mambo mawili. Kwanza, Malkia alimpokea Mzee Mkulima kila waliporudi. Malkia alichukua chakula chote na kukipeleka jikoni. Paka aliona kuwa, Malkia humpokonya Mzee Mkulima chakula chote bila mzee kusema chochote.

Pili, Mzee Mkulima hakuwahi kumpa paka chakula wakiwa shambani. Hata hivyo, kila mara Malkia alipopika chakula, alikuwa akimpa paka chakula kingi. Mambo haya mawili yalimfanya paka ampende Malkia zaidi ya Mzee Mkulima.




Baada ya siku kadhaa, paka alichoka kwenda shambani na Mzee Mkulima.

Aliona ni bora kukaa jikoni na Malkia. Akawa rafiki ya Malkia.

Paka akawa hatoki jikoni tena.

Mzee Mkulima alisikitika sana kwa kukosa rafiki wa kwenda naye shambani.

Siku moja akamwita paka na kumuuliza, "Rafiki yangu, kwa nini siku hizi hutaki kwenda shambani na mimi?" Paka alimjibu, "Mzee, mimi sikujua una uchoyo na woga hivyo. Tukienda shambani sote, hunipi chakula chochote. Tunapofika nyumbani, mama hukupokonya chakula chote na hata husemi kitu. Mama akitayarisha chakula, hunipa, nala hadi nashiba."



Paka aliendelea, “Kwa hivyo mzee, mimi siendi na wewe shambani tena. Mimi nitakaa na mama jikoni. Siwezi kwenda shambani na mtu mchoyo na mwoga kama wewe.”

Kuanzia siku hiyo, urafiki wa paka na Mzee Mkulima uliisha.



Paka akahamia jikoni mpaka leo.

## Maswali


1. Mke wa Mzee Mkulima aliitwa nani?
2. Taja mambo mawili ambayo yalimshangaza paka.
3. Kwa nini paka alimpenda Malkia zaidi ya Mzee Mkulima?

# Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu

*Mwandishi:* ***Stephen Kwoma***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

Hapo kale wanyama waliishi pamoja. Kila mnyama alimpenda mwenzake. Sherehe zote walifanya pamoja.



Siku moja, Sungura aliwaalika wanyama kwa harusi ya binti yake. Wanyama hawa walifurahia sana mwaliko huo. Hivyo basi, wanyama walijiandaa kwa kila namna ili kuhudhuria harusi hiyo.

Wanyama walinunua nguo nzuri nzuri. Wengine waliomba mavazi kutoka kwa marafiki zao. Twiga alienda kuomba mkufu kutoka kwa Swara. Swara alisita kumpa Twiga mkufu. Mwishowe Swara akakubali kumpa mkufu.

Siku ya harusi ilipofika, wanyama walivalia mavazi yao ya kupendeza. Twiga naye aliuvaa mkufu aliouomba kutoka kwa Swara.


Twiga alipendeza mno mpaka kila mnyama akautamani ule mkufu wake.



Harusi yenyewe ilikuwa ya kufana sana. Wanyama walikula vyakula vitamu na kucheza densi. Sungura alifurahia kufika kwa wanyama wenzake. Aliwashukuru kwa kufika katika harusi ya bintiye.


Sherehe zilipoisha, kila mnyama alienda zake kupumzika. Twiga naye alitorokea msituni na ule mkufu wa Swara.

Swara alimsubiri Twiga arudishe mkufu wake lakini wapi! Siku iliyofuata, Swara alimwendea Mfalme Ndovu na kumshtaki Twiga. Ndovu aliwaita wanyama wote na kuwaamuru wamtafute Twiga.



Twiga alipopatikana, alifikishwa mbele ya Mfalme Ndovu. Wanyama walijaribu kumvua ule mkufu lakini hawakuweza.

Waliposhindwa wakapendekeza mbinu tofauti za kuuvua ule mkufu. Sungura alisema, "Tumfunge kisha tumchape." Mfalme Ndovu alikataa wamchape Twiga. Chui naye akasema, "Tumfunge kamba kisha tuuvute mkufu kwa nguvu." Wanyama wengi walionekana kufurahia pendekezo hilo.



Twiga alifungwa kamba kisha Ndovu akauvuta mkufu kwa kuutumia mkonga wake.

Vile Ndovu alivyouvuta mkufu ndivyo shingo ya Twiga ilivyoendelea kuwa ndefu.

Hatimaye, mkufu ulitoka lakini shingo ya Twiga ikawa ndefu. Kwa hivyo Twiga aliona aibu akatorokea msituni.

## Maswali

1. Wanyama walialikwa kwa sherehe ya harusi ya nani?
2. Twiga alimuomba Swara nini?
3. Kwa nini Swara alimshtaki Twiga kwa Mfalme Ndovu?
4. Ni nani aliyewaambia wanyama wauvute mkufu?
5. Ni nani aliyevuta mkufu kutoka shingoni mwa Twiga?

**Darasa la 2**

Kitabu cha hadithi 4

# ☆ Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni

# ☆ Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

Darasa la 2

Kitabu cha hadithi 5

Kiswahili

# ★ Safari ya Mombasa

# ★ Masaibu ya Musa



Tusome Early Literacy Programme

# Safari ya Mombasa

*Mwandishi:* ***Nashera Ara Kodawa***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***

“Amina!” Mamake Amina alimwita. “Umeshapanga vitu vyako? Fanya haraka usichelewe.”

“Ndiyo mama, kila kitu kimepangwa,” Amina alimjibu.

Amina na binamu yake walikuwa wamepanga kwenda Mombasa. Mipango yote ilikuwa imekamilika.

Mara mlango ulibishwa. Amina alikimbia kuufungua. Alikuwa Sifa, mjomba wake Amina. Amina alimrukia na kumkumbatia, “Mjomba Sifa! Karibu sana!”

“Mko tayari? Twende, muda wetu umeisha,” mjomba alisema.

Sifa akamsalimia mama yake Amina. Kisha wakaondoka kwenda katika stesheni ya garimoshi. Kulikuwa na msongamano mkubwa wa magari barabarani. Sifa akasema, “Amina, leo mtaachwa na garimoshi.”



“Tafadhali mjomba usiseme hivyo,” Amina alilalamika.

Walifika katika stesheni ya garimoshi ya Nairobi na kupanda garimoshi. Walikuwa Amina, Asha, Kadogo na Saidi.

Baada ya muda mfupi, garimoshi liliondoka kwenye stesheni kwa mwendo wa kasi.

"Lo! Karibu tuchelewe," Amina alisema. Walimpa mjomba Sifa kwaheri kwa kumpungia mkono wakiwa na furaha tele.



Gari lilipofika Athi River watoto hao walifurahi kuona maeneo tofauti. Waliona kituo cha kuchinjia ng'ombe.

"Tucheze mchezo wa kadi!" Alisema Saidi. Saidi alikuwa mkubwa wa watoto hawa wote. Walifurahishwa sana na mchezo wa kadi. Walitumia wakati huu pia kuzungumzia yale watakayofanya watakapokuwa Mombasa.

Mara, mhudumu wa hoteli alipita na kuwaambia kuwa chakula cha jioni kilikuwa tayari.

"Ni furaha iliyoje kula chakula katika hoteli ndani ya garimoshi.

“Ni muhimu garimoshi kuwa na mkahawa ndani. Hii ni kwa sababu linapitia kwenye sehemu ambazo watu hawawezi kupata chakula.

Garimoshi pia husimama katika vituo maalumu pekee. Kwa hivyo haliwezi kusimama kama basi ili abiria wanunue chakula,” alisema Sifa.



“Isitoshe, safari ya garimoshi huchukua muda mrefu sana njiani.”

"Hivyo, abiria wanahitaji chakula ili wasiwe na njaa," aliendelea Sifa.

"Ni kweli, ikiwa hapangekuwa na mkahawa ndani ya garimoshi, tungefika Mombasa tukiwa na njaa tele," alisema Asha.

Baada ya chakula, watoto walilala usingizi mzito. Walipoamka, gari lilikuwa limefika Mariakani. Walipiga meno mswaki, wakanawa uso na kuelekea hotelini kupata kiamshakinywa.

"Tuanze kupanga mipango ya leo," Amina alisema.

"La! Kwanza tumpigie shangazi simu tumwambie tunaelekea Mazeras," alisema Saidi.

Walimpigia shangazi yao simu akawaeleza kuwa wangempata kwenye stesheni Mombasa. Waliposhuka katika stesheni, shangazi yao aliwapokea na kuwapeleka nyumbani.
Baada ya kuoga waliondoka kwenda kuzuru Fort Jesus.



Huko Fort Jesus waliona ngome ya zamani sana. Ndani ya ngome hiyo waliona pia vitu vya zamani sana.


“Njoo Saidi! Njoo uone sanamu za Waswahili na vyombo walivyotumia zamani.”

Waliona pia kisima cha zamani sana ambacho kilitumiwa na Wareno.



Ilipofika saa saba na nusu, walienda kula chakula cha mchana na kuelekea sehemu iitwayo Bamburi Nature Trail kwa matembezi mwituni.

“Leo nataka nimpige picha yule kobe mwenye miaka zaidi ya mia moja,” Amina alisema. Kila mmoja wao alipigwa picha na huyo kobe.



Waliporudi nyumbani shangazi yao aliwaandalia chakula mapema.

“Nataka mle mapema ili muweze kulala mapema. Najua mmechoka sana,” shangazi yao aliwaambia.

Wakati wa chakula walizungumza juu ya yale waliyoona huko Fort Jesus na Bamburi Nature Trail.

"Haya! Laleni mapema ili kesho muwe wachangamfu." Shangazi yao aliwaambia. Usiku huo watoto wote walilala fo fo fo!

## Maswali

1. Amina na binamu yake walipanga kwenda wapi?
2. Ni nini kingefanya Amina waachwe na garimoshi?
3. Watoto walifurahia kuona nini Athi River?
4. Watoto walifanya nini baada ya kula chakula?
5. Baada ya kuoga, watoto walienda wapi?

# Masaibu ya Musa

*Mwandishi:* ***Nashera Ara Kodawa***

*Mchoraji:* ***Bonface Andala***


Musa alikuwa mvulana wa darasa la pili. Hakuwa amewahi kuendesha gari tangu alipozaliwa. Musa alikuwa akiangalia kila kitendo ambacho baba yake alikifanya alipokuwa akiendesha gari akimpeleka shuleni. Aliangalia jinsi baba yake alivyoingiza ufunguo mahali pake. Alitazama pia alivyoweka gia na kuzibadilisha. Asubuhi moja baba yake akimpeleka shuleni kama kawaida, Musa alifanya kitendo cha ajabu sana.



Baba yake Musa aliegesha gari kando ya barabara na kuingia dukani. Alitaka kumnunulia Musa daftari la mazoezi ya hesabu. Kwa haraka, Musa aliondoka kwenye kiti chake na kukikalia kiti cha dereva.

Baba yake alikuwa amesahau ufunguo wa gari. Musa alizungusha ufunguo na gari likanguruma.

Baada ya gari kunguruma, Musa alitoa breki ya mkono na kuweka gia ya kwanza. Gari lilianza kwenda. Mara Musa alishikwa na woga. “Gari laondoka! Nitalisimamisha vipi? Nilikuwa ninajaribu tu…” Musa aliwaza. Alimwona baba yake akitoka dukani akajua mambo yameharibika. Alijaribu kulisimamisha gari lakini hakufaulu. Gari liliendelea kuongeza kasi. Musa alijaribu kila aliloliwaza lakini yote hayakumsaidia. Moyo ulimdunda sana. Alihepa kwa karibu sana kugongana na pikipiki moja.



Musa alisikia honi za magari kila upande huku wengine wakimpita na kumtusi. Alitokwa na jasho mwili mzima. Gari lilifika kwa barabara kuu na hata kuongeza kasi zaidi.

Aliwaza sana jinsi ya kulisimamisha gari hilo lakini hakupata la kumsaidia. Kwa bahati ilikuwa asubuhi sana na kwa hivyo hapakuwa na magari mengi barabarani.

Alifikia kivukio cha wanaotembea kwa miguu. Akakumbuka kupiga honi. Alipiga honi kwa mfululizo. Wanafunzi waliokuwa wakivuka walikimbilia kando ya barabara. Wakati huu gari lilianza kuyumbayumba. Alitoa mkono mmoja nje na kupiga honi. Madereva wengi walitoka barabarani na kumpa nafasi.



Mara baba yake alifika kando ya dirisha la gari akiwa juu ya pikipiki. Kumbe alikuwa amemfuata kwa pikipiki. "Musa! Umefanya nini? Utasababisha ajali! Simamisha gari!" Mara polisi wa pikipiki alifika na kushangaa kuona dereva aliyevalia sare ya shule.

Alishangazwa zaidi alipoona ni mwanafunzi mdogo wa shule.



Kwa bahati nzuri, katika hali za kutafuta suluhisho, Musa aliisongesha gia na gari lilipunguza mwendo. Lilitembea taratibu hadi lilipogonga jiwe kando ya barabara na kusimama. Taa za gari zilivunjika. Musa alipata majeraha kwenye miguu.

Alishtuka sana hata hakujua alichofanya ili gari lisimame. Polisi na baba yake wakawa pia wameegesha pikipiki zao. Yule polisi alimkaribia Musa kwa hasira lakini baba yake akamtuliza. Akamwambia polisi kwamba yeye ndiye aliyekuwa mwenye gari. Polisi alikuwa amedhani kuwa Musa alikuwa ameiba gari hilo.

Baba yake Musa alimwomba yule polisi msamaha. "Nakubali mimi ndiye mwenye makosa, nilisahau ufunguo ndani ya gari, tafadhali nisamehe," babake Musa alimsihi polisi. Mwishowe polisi alikubali kumsamehe.

“Mwanangu Musa nitajua la kumfanyia tutakapofika nyumbani,” baba yake Musa alimweleza polisi.

Wakati huu wote, Musa alikuwa akitetemeka sana huku jasho likimtoka mwili mzima. Musa alimuomba baba yake msamaha.

Kabla ya kumsamehe, baba yake Musa alimuonya asirudie makosa hayo tena. Alimwambia ya kwamba alihatarisha maisha yake na ya watumiaji barabara wengine. Babake alimpeleka Musa hospitali. Alipewa dawa na kudungwa sindano.

Walipofika nyumbani, babake akamwambia kwamba hangemruhusu kumtembelea mjomba wake. Hii ilikuwa adhabu kwa Musa. Musa alikuwa akitarajia kumtembelea mjomba wake shule ikifungwa. Mjomba wake aliishi jijini. Tangu siku hiyo, Musa hakuwahi kurudia makosa kama yale.

## Maswali

1. Musa alikuwa katika darasa gani?
2. Babake Musa alitaka kumnunulia Musa nini?
3. Kwa nini Musa alitokwa na jasho mwili mzima?
4. Baba yake Musa alimfanya nini baada ya kosa?

# Darasa la 2

**Kitabu cha hadithi 5**

## ★ Safari ya Mombasa

## ★ Masaibu ya Musa

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.